SEKTA YA MAENDELEO YA JAMII

1:0 UTANGULIZI

Idara ya Maendeleo ya Jamii,Ustawi wa Jamii na Vijana Wilayani Mbinga kwa kushirikiana na Wadau wa Maendeleo wa ndani na nje ya Halmashauri inaendelea kutoa huduma bora na endelevu kwa Wananchi wake kwa kuzingatia vipaumbele vilivyopo kwa kufuata kanuni, sheria, taratibu za ushirikishwaji, uwajibikaji na Utawala bora.

Idara ya Maendeleo ya Jamii, Ustawi wa Jamii na Vijana inatekeleza kazi yake kwa kuzingatia mapendekezo ya mipango shirikishi jamii kwa kutumia fursa na vikwazo kwa maendeleo, mipango hiyo inashirikisha vijiji na kata, wataalamu, kutoka nyanja zote, wadau wa Maendeleo, maelekezo na maagizo ya Serikali juu ya MKUKUTA, MKURABITA, hifadhi ya mazingira, azimio la kilimo kwanza, ikijumuisha ilani ya uchuguzi ya CCM ya mwaka 2010

2:0 SERA NA SHERIA ZILIZOKUWA ZINAONGOZA SEKTA YA MAENDELEO YA JAMII

2:1 SERA

Idara ya Maendeleo ya Jamii imekuwa ikiongozwa na Sera Mama ya Tanzania ambayo ni Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea.Chimbuko la Sera hii ni Azimio la Arusha la

mwaka 1967.Mnamo mwaka 1996 Sekta ya Maendeleo ya Jamii imekuwa ikitekeleza majukumu yake kwa kuongozwa na Sera ya Maendeleo Jamii ya mwaka 1996.Sera hii inatoa maelekezo ya namna ya kutekeleza shughuli za kila siku za kimaendeleo kwa jamii na kuonyesha bayana wajibu wa wahusika mbalimbali katika kuharakisha maendeleo ya jamii nchini.

2.2 SHERIA

Baadhi ya sheria ambazo zimekuwa zikisimamiwa na kutekelezwa na idara ya maendeleo ya jamii ni kama vile sheria ya UKIMWI ya mwaka 2008 na sheria ya watoto ya mwaka 2009 .Sheria hizi zinalenga kusimamia kikamilifu ustawi wa watoto na mapambano dhidi ya UKIMWI.

3:0 MATUKIO MAKUU KATIKA MFUMO WA SIASA, ULINZI, UTAWALA, KIUCHUMI, KITEKNOLOJA NA KIJAMII.

3:1 MFUMO WA SIASA

Sekta ya Maendeleo ya Jamii ikiwa ni sehemu za sekta mojawapo katika Serikali ya Tanzania zao la Siasa Mama ya Ujamaa na Kujitegemea ambayo iliasisiwa na Mwasisi wa Taifa hili Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kupitia Azimio la Arusha mwaka 1967.Mnamo mwaka 1992 Tanzania iliingia katika mfumo wa Soko Huria, ambapo

sekta binafsi zilipewa kipaumbele katika kutekeleza shughuli mbalimbali za maendeleo .Pia Tanzania katika kipindi hiki iliingia katika mfumo wa vyama vingi vya siasa.

3:2 UTAWALA

Katika kipindi cha miaka 50 ya Uhuru Tanzania imepitia katika awamu nne za uongozi kuanzia Mwasisi wake Hayati Mwalimu Julius K. Nyerere(1961-1985), Rais Mstaafu Alli Hassan Mwinyi (1985-1995) Rais Mstaafu Benjamin William Mkapa (1995-2005) na kwa kipindi hiki Rais wa Tanzania ni Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete. Pia Tanzania lina Bunge ambalo wabunge wake wanatoka katika vyama mbalimbali vya siasa.

3:3. KIUCHUMI

Kiuchumi, Idara ya Maendeleo ya Jamii inasimamia na wananchi kujiletea maendeleo yao wenyewe kwa kuiwezesha jamii kuibua , kupanga na kutekeleza mipango ya maendeleo yao.Aidha wananchi kwa kupitia vikundi vya kiuchumi au mwananchi mmoja mmoja wanatakiwa kutumia fursa za kimaendeleo zilizopo katika maeneo yao ili kujiletea maendeleo yake mwenyewe, familia na Taifa kwa ujumla.

3:4. KITEKNOLOJIA

Sekta ya maendeleo ya Jamii imekuwa ikisimamia na kuwawezesha wananchi kutumia teknolojia rahisi za ujenzi na nyumba bora kupitia vikosi vya ujenenzi vijijini na teknolojia inayosaidia kumpunguzia mama mzigo wa kazi kama vile majiko sanifu.Pia mkazo umewekwa katika teknolojia inayopunguza athari ya uharibifu wa mazingira kwa kuhimiza matumizi ya nishati mbadala-kama vile matumizi pumba katika kuchomea matofali.

3:5. KIJAMII

Idara ya Maendeleo ya Jamii, Ustawi wa Jamii na Vijana imejikita sawia katika kuisaidia jamii kuepukana na maambukizi mapya ya VVU/UKMWI. Katika harakati za kutekeleza Mkakati wa Pili wa Taifa wa kupunguza maambukizi mapya ya VVU/UKIMWI Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga kupitia kitengo cha UKIMWI (W) na Kamati ya Kudhibiti UKIMWI (W) imetekeleza shughuli zifuatazo kwa umakini mkubwa:-

- Upimaji wa VVU/UKIMWI kwa hiari kwa kipindi cha 2005/2011 wenye jumla ya Wananchi wapatao 90,292.
- Wananchi wenye maambukizi kwa kipindi cha 2005/2011 ni 5602
- Wananchi wanaotumia dawa za kufubaza (ARVs) ni 3501

- Msaada kwa Watoto Yatima ngazi ya Sekondari wapatao 900 ni Tshs 44,370,000/=
- Huduma kwa Watumishi 50 wanaoishi na VVU/UKIMWI ni Tshs 12,060,000/=
- Msaada kwa makundi tete (SHIDEPHA) vikundi vipatavyo 15 vimepatiwa jumla ya Tshs 7,500,000/=

4:0 **MAFANIKIO**:

4:1 **MAFANIKIO-VIKOSI VYA UJENZI**:

- Uanzishwaji wa vikosi vya ujenzi 229 vya ufundi, uashi na uselemala.
- Uanzishwaji vikosi 49 vya uhunzi
- Uanzishwaji wa vikosi 69 vya ufundi bomba vikosi hivyo katika ngazi ya vijiji.

4:2 **VIKUNDI VYA WANAWAKE /VIJANA**:

- Idara imefanikiwa kuwezesha kuanzisha vikundi 1,110 vya wanawake na kupatiwa mtaji wa Tshs 96,050,000/=
- Idara imefanikiwa kuwezesha kuanzisha vikundi vya kiuchumi vya vijana vipatavyo 810 katika Kata 49
- Vikundi 2 vya vijana kupitia SACCOS ya Ruhehei na Hagati vimewezeshwa kupata mikopo ya Tshs

10,000,000/= kwa mwaka wa fedha 2009/2010 ilikuwasaidia kuanzisha shughuli za ujasiliamali,.

- Kupitia mpango wa uwezeshaji vijana (YEP) Vijana wameweza kuanzisha kituo cha Vijana kwa usimamizi wa Idara ya Maendeleo ya Jamii (Kituo kipo Mbinga mjini).
- VICOBA 74 vinaendelea kutoa taarifa zake za hisa, uanachama na Miradi yao. Jumla ya Tshs.35,050,000/=zimekusanywa kama hisa zao chini ya uratibu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii, Ustawi wa Jamii na Vijana (W).

4:3.UIMARISHAJI WA MAHUSIANO KATI YA HALMASHAURI, ASASI ZA KIRAIA NA WANANCHI

- Kuna asasi za kiraia za ndani ya wilaya zipatazo 54 na zile za nje ya wilaya zipatazo 5.
- Idara imewezesha wananchi kuanzisha vikundi vya kijamii vinavyojishughulisha na shughuli za kiuchumi vipatavyo 569.
- Idara imefanikiwa kutoa hati za usajili wa ndani (kiwilaya) kwa vikundi vya kijamii vinavyojishughulisha na shughuli za kiuchumi vipatavyo 569.
- Halmashauri kupitia Idara ya Maendeleo ya Jamii imefanikiwa kutoa mchango wa Tshs 5,000,000/= kwa ajili ya kusaidia Wazee kupitia Asasi ijulikanayo kama SAIDIA WAZEE yenye makao makuu Mbinga Mjini.

- Idara imefanikiwa kuwatambua Walemavu wa ngozi (Albino) na kuwapatia msaada wa Tshs 2,735,000/= kwa ajili ya matibabu na kuwajengea uwezo Kiuchumi.
- Halmashauri kwa kushirikiano na Mtandao wa Asasi za kiraia ndani ya wilaya-
  (MBINGONET) imefanikiwa kuandaa kongamano la pamoja kati ya Asasi za kiraia ili kubadilishana uzoefu na kuweka mikakati ya pamoja katika mapambano dhihi ya VVU/UKIMWI na Umaskini.

4:4 UIMARISHAJI WA DAWATI LA JINSIA:

- Idara imefanikiwa kuanzisha dawati la Jinsia linalojishughulisha na kutatua migogoro ya wanandoa na kusaidia kuzitambua haki za Wanafamilia.
- Idara imetoa mafunzo ya masuala ya Jinsia katika mipango ya maendeleo kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii 20 ili kuwapa uwezo wa kiutendaji katika maeneo yao ya kazi. Jumla ya Tshs.4,578,000/=.zilitumika kwa kutekeleza mafunzo hayo.
- Vikundi 29 vya wanawake vimeanzishwa na kupata elimu ya ujasiriamali.

5:0 FURSA ZILIZOPO:

- Uwepo wa watumishi wa Sekta ya Maendeleo ya Jamii katika ngazi ya wilaya na kata yenye Jumla ya Watumishi 34 wenye ujuzi na uzoefu kazini.
- Uwepo wa wananchi wapatao 356,223 wenye uwezo na juhudi ya kufanya kazi kwa ajili ya kujiletea maendeleo katika maeneo yao.
- Uwepo wa Asasi za kijamii na kiraia (NGOs na CBOs) zipatazo 628 ambazo zinatoa mchango mkubwa katika kuhamasisha na kuelekeza wananchi kuhusu masuala mbalimbali ya kijamii, kiuchumi, mazingira na ki`teknolojia.
- Uwepo wa ardhi yenye rutuba. Ipatayo 5391 SQ KM
- Uwepo wa vyanzo vya maji vyenye ukubwa wa 3979 SQ KM
- Uwepo wa misitu wenye ukubwa wa eneo 2526 SQ KM
- Mvua ya kutosha yenye ujazo wa mm 1200 .
- Uwepo wa Asasi ndogondogo za kifedha zinazotoa huduma za kifedha kwa jamii kama vile; SACCOS na VICOBA.
- Uwepo wa Taasisi kubwa za kifedha zinazotoa huduma za kifedha kwa jamii kama vile NMB, CRDB na Mbinga Community Bank.
- Uwepo wa miundombinu ya mawasiliano na usafirishaji kama vile Simu, Internet, Barabara na Bandari ndogo.

- Uwepo wa Taasisi mbalimbali zinazotoa huduma kwa wananchi kama vile, Hospitali, Shule za Msingi na Sekondari, Zahanati, Vituo vya Afya na Vyuo vya Ufundi.
- Uwepo wa utawala bora na unaojali, kanuni sheria na taratibu katika ngazi za Vijiji, Vitongoji, Kata hadi Wilaya.

6:0 CHANGAMOTO

- Ufinyu wa bajeti katika kutekeleza majukumu.
- Upungufu wa watumishi kada ya Maendeleo ya Jamii hususani katika ngazi ya kata na vijiji.
- Upungufu wa vitendea kazi kama vile vyombo vya usafiri na kompyuta katika ngazi ya Kata.
- Uwingi wa NGO's/CBO's zisizokuwa na uwezo/mitaji ya kusaidia wananchi kutumia fursa zilizopo.
- Baadhi ya NGO's /CBO's kutokuwa na mipango thabiti ya uendeshaji na upatikanaji wa rasilimali watu na fedha ili kumudu kutekeleza mipango yao.
- Baadhi ya Sekta nyingine kuto tambua umuhimu wa Sekta ya maendeleo ya Jamii katika kuraghibisha mipango ya maendeleo kwa wananchi.

7. MATARAJIO KATIKA MIAKA 50 IJAYO

- Kuifanya sekta ya Maendeleo ya Jamii kuwa kiongozi wa sekta zote katika kuiwezesha Jamii kupanga,

kusimamia, kutekeleza na kufanya tathmini ya miradi yote ya maendeleo.

- Kuwa na Maafisa Maendeleo ya Jamii katika ngazi ya vijiji na kata ili kuharakisha maendeleo.
- Kuelimisha jamii ili kuwa na familia bora yaani kupunguza migogoro katika familia ili kupunguza tatizo la watoto wa mitaani.
- Kuwa na vitendea kazi vya kutosha na vinavyokidhi haja ili kuboresha utekelezaji wa majukumu ya kila siku ya idara.
- Kuiwezesha Jamii kuzielewa Sera mbalimbali zilizopo na zinazotekelezwa katika kuongoza na kuelekeza shughuli za maendeleo ya Jamii zilizoibuliwa katika kwa mpango shirikishi jamii.
- Kuimarisha mfuko wa wanawake na vijana ili uweza kukidhi mahitaji ya walengwa kwa maslai ya Taifa.

Katika kuharakisha Maendeleo ya Jamii, Sekta ya Maendeleo ya Jamii, Ustawi wa Jamii na Vijana ina jukumu kubwa sana la kupiga msasa kwa wananchi ili waweze kujitolea na kushiriki kikamilifu katika kutekeleza mipango ya maendeleo waliyojipangia wenyewe kwa kutumia njia ya fursa na vikwazo kwa maendeleo ya mwaka 2002, haya yanawezekana tunahitaji uthubutu.